Jarida la
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
TOLEO MAALUM NA. 020

# TOLEO MAALUM

## MAADHIMISHO YA MAONESHO YA NANENANE

88 2024

# Jiji la Dodoma kidedea Maonesho ya Nanenane 2024











**"Chagua viongozi bora wa serikali za mitaa kwa maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi"**

# BODI YA UHARIRI


## MWENYEKITI

**Bw. John Kayombo**
Mkurugenzi
Halmashauri ya Jiji la Dodoma

## MHARIRI WA HABARI

**Bw. Dennis Gondwe**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Jiji la Dodoma

## WAJUMBE

**Bi. Francisca Mselemo**
Afisa Habari
Halmashauri ya Jiji la Dodoma

**Bi. Theresia Nkwanga**
Afisa Habari
Halmashauri ya Jiji la Dodoma

## MSANIFU JARIDA

**Bw. Emmanuel Lucas**

# Jiji la Dodoma kidedea Maonesho ya Nanenane 2024

Na. Dennis Gondwe

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma kinara wa tuzo na zawadi mbalimbali kwenye maonesho ya kimataifa ya Nanenane kutokana na kufanya vizuri katika maeneo mengi na kuwa kivutuo kwa wageni waliotembelea maonesho hayo.




*Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi mfano wa ufunguo wa Trekta mkulima Dafalah S. Wadaa, Mkulima bora wa Kanda Kitaifa aliyezawadiwa Trekta na Bodi ya Pamba*

Katika tuzo na zawadi zilizotangazwa mbele ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Halmashauri ya Jiji la Dodoma iliibuka mshindi katika vipengele sita vya mashindano ya Nanenane. Katika kipingele cha zawadi za wakulima bora kitaifa, Kanda ya Kati iliyotolewa na Bodi ya Pamba, Dafalas Wadaa kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma alizawadiwa zawadi ya Trekta. Kipengele cha wafugaji bora, mshindi wa kwanza aliibuka John Nassar kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma na kuzawadiwa mitamba wawili yenye thamani ya shilingi 9,000,000, mashine ya kukamua yenye thamani ya shilingi 2,300,000 na fedha taslimi shilingi 18,700,000. Maeneo mengine ambayo Halmashauri ya Jiji la Dodoma iliibika kidedea ni eneo la wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa ambapo wafugaji John Nassar aliibuka mshindi wa kwanza na kupata zawadi ya shilingi 2,500,000 na Viola Kweka, mshindi wa pili na kupata zawadi ya shilingi 2,000,000. Kwa wafugaji wadogo wa mbuzi wa nyama, Venderine Liakurwa pia wa Dodoma Jiji aliibuka mshindi wa pili na kupata zawadi ya shilingi 1,000,000. Eneo la wafugaji wadogo wa mbuzi wa maziwa, Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilitoa washindi wa kwanza na wa pili mtawalia. John Nassari aliyepata zawadi ya shilingi 1,500,000 na Caroline Shayo aliyepata shilingi 1,000,000.

Kwa washindi katika mikoa ya Dodoma na Singida, Halmashauri ya Jiji la Dodoma iliibuka kidedea kwa kushika nafasi ya kwanza ikizitangulia Halmashauri za Wilaya ya Kondoa na Mpwapwa za Mkoa wa Dodoma.

Maonesho ya Nanenane mwaka 2024 yaliongozwa na kaulimbiu isemayo "Chagua viongozi bora wa serikali za mitaa kwa maendeleo endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi".

"Chagua viongozi bora wa serikali za mitaa kwa maendeleo endelevu ya kilimo, mifugo na uvuvi"

# Viongozi wamshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kukuza sekta za Mifugo na Uvuvi

Na. Flora Nadoo

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti amshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kuzipa kipaumbele sekta za mifugo na uvuvi ili zichangie katika uchumi wa taifa.



*Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan (picha na maktaba)*

Shukrani hizo alizitoa wakati akitoa salamu za Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika uzinduzi wa maonesho ya Nanenane yanayofanyika katika viwanja vya Nanenane Nzuguni Dodoma.

Mnyeti alisema "Mheshimiwa Rais ameongeza bajeti ya wizara yangu kutoka shilingi bilioni 295.9 mwaka 2023/2024 hadi shilingi bilioni 460.3 kwa mwaka 2024/2025 sawa na nyongeza ya 50.5%. Fedha hizi zitatumika katika kuimarisha sekta ya mifugo na uvuvi na kuongeza mchango wake katika pato la taifa.

Pia Waziri wa Kilimo Husein Bashe alimshukuru mgeni rasmi Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa kutenga muda wake na kuifanya kazi hiyo. Awashukuru kwa mchango wao mkubwa sana kwenye kilimo.

Hivyo basi, Husein Bashe alimshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294.97 mwaka 2021/2022 hadi kufikia bajeti iliyopitishwa tarehe 7/6/2024 shilingi trilioni 1.2. Fedha hizo zilizoongezeka zitatumika kwenye kilimo. Pia aliishukuru serikali kutenga fedha kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kutokana na mchango wa serikali kwenye kilimo, imepelekea uzalishaji mkubwa sana wa mazao. Aidha, mchango huo umewezesha kufanikisha kupeleka mahindi nchini Zambia kama ilivyokuwa imesainiwa. Mahindi hayo ni jumla ya tani 600,000. Pia kwa mara ya kwanza NFRA imeuza mahindi kwa dola ambayo ni historia ya nchi yetu. NFRA imefungua vituo vya kununua mahindi. Vivyo hivyo, serikali inatoa ruzuku kwenye pembejeo na kwenye bei ya kununua mazao, ili kuwasaidia wakulima na kuwawekea mazingira bora, aliongeza. Alimalizia kwa kusema kuwa serikari yaahidi kwamba hakuna mkulima yeyote wa mahindi ambaye atakosa sehemu ya kuuza mahindi yake. Serikali itanunua mahindi yote yaliyo mikononi mwa wakulima.

"Mheshimiwa Rais ameongeza bajeti ya wizara yangu kutoka shilingi bilioni 295.9 mwaka 2023/2024 hadi shilingi bilioni 460.3 kwa mwaka 2024/2025 sawa na nyongeza ya 50.5%. Fedha hizi zitatumika katika kuimarisha sekta ya mifugo na uvuvi na kuongeza mchango wake katika pato la Taifa"

# Uwanja wa Maonesho wa Nanenane Nzuguni-Dodoma wafurika



Na. Flora Nadoo

UWANJA wa maonesho ya Nanenane Kanda ya Kati, Dodoma wafurika watu kutoka sehemu mbalimbali kwa ajili ya kushuhudia ufunguzi huo.

Mbali na ufunguzi huo wa maonesho ya Nanenane, wananchi washuhudia uzinduzi wa Tukutuku (Pikipiki za miguu mitatu) takribani 100 ambazo zitagawiwa kwa vijana. Kupitia pikipiki hizo vijana watapata faida kubwa sana kwasababu ni pikipiki zilizotengenezwa kisasa zaidi na hivyo, zitakuwa zinatoa kahawa ya viwango vya juu sana.

Kwa upande wa burudani, wananchi walifurahia sana wagogo wakicheza ngoma zao za asili kwa umahili mkubwa wakiongozwa na mwalimu wao aliyefahamika kwa jina la Malima.

Kutokana na kufurika kwa watu hao, watu wenye vyombo vya moto kama bajaji, pikipiki na magari wajipatia faida kubwa tofauti na siku zote kufuatia kutoa huduma ya usafiri.

# RC aishukuru serikali kupeleka Nanenane kitaifa Dodoma

Na. Fadiga James

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule ameishukuru serikali kwa kuamua maonesho ya Nanenane kitaifa kufanyikia Dodoma na kusema ni fursa kwa wananchi wa mkoa huo kunufaika kiuchumi.




Senyamule alitoa shukrani hizo wakati akitoa salamu za Mkoa wa Dodoma kwenye ufunguzi wa maonesho ya Nanenane kitaifa yaliyofanyika Kanda ya Kati uliofanywa na Waziri Mkuu wa Tanzania katika viwanja vya Nanenane, Nzuguni jijini Dodoma.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ameishukuru serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha sherehe za Nanenane kufanyika jijini Dodoma na kusema kuwa ni mahali sahihi kwasababu wakulima na wafugani ni wengi na zitasaidia wananchi kukua kiuchumi.

"Kipekee nishukuru sana kwa dhati kuwa mwaka huu 2024 maonesho ya Nanenane yanafanyika Kanda ya Kati kitaifa katika Mkoa wa Dodoma. Tunashukuru sana kwasababu ni historia ya muda mrefu kidogo, tulishaanza kusahau kuandaa hata haya maonesho ya kimataifa, lakini tutoe shukrani nyingi kwa mheshimiwa Rais, lakini tutoe shukrani nyingi kwa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa uamuzi huu" alisema Senyamule.

Alitumia ufunguzi huo kuwataka wakazi wa Dodoma kuchangamkoa fursa ya maonesho hayo kufanyikia Dodoma kukua kiuchumi.

# Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aweka jiwe la msingi kiwanda cha kuunganisha Matrekta jijini Dodoma

Na. Dennis Gondwe

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka jiwe la msingi kiwanda cha kuunganisha matrekta na zana nyingine za kilimo kwa lengo la kusogeza matumizi ya matrekta karibu na wakulima nchini na kuwapunguzia gharama.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka jiwe la msingi kiwanda cha kuunganisha matrekta*

Jiwe hilo la msingi liliweka na Rais katika viwanja vya Nanenane, Nzuguni jijini Dodoma.

Akitoa maelezo ya awali, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema kuwa kiwanda cha kuunganisha matrekta na zana nyingine za kilimo ni ushirikiano wa kampuni ya Agricom na Mahindra kutoka nchini India. Alisema kuwa makubaliano baina ya wizara yake na Mwenyekiti wa taasisi ya sekta binafsi nchini, Angelina Ngalula ni kuwa kampuni hizo kufikia mwezi Juni, 2025 kiwanda hicho kianze kutoa huduma.

Aidha, kiwanda cha kuunganisha matrekta kinajengwa katika viwanja vya Nanenane, Nzuguni Dodoma eneo lenye ukubwa wa mita za mraba takribani 20,0000 kikiunganisha matrekta aina na Swaraj na kutarajiwa kuzalisha ajira za kudumu 400 na ajira zisizo za kudumu zaidi ya 2000.

Ikumbukwe kuwa uwekezaji wa kiwanda hicho ni matokeo ya ziara ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan nchini India na kualika wawekezaji wa India kuwekeza nchini Tanzania pamoja na mambo mengine.

# PM azindua Pikipiki za miguu mitatu kuwawezesha vijana

Na. Flora Nadoo

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa amezindua zoezi la usambazaji wa pikipiki za miguu mitatu 100 kwa ajili ya vijana katika viwanja vya Nanenane jijini Dodoma.

Alisema kuwa pikipiki hizo zitatolewa kwa mkopo nafuu sana na marejesho hayatakuwa na riba yoyote. "Pikipiki hizi zina mashine ya kusagia kahawa, sehemu za kukaa watu kwa ajili ya kusambaza kahawa" alisema Waziri Bashe.

Shirika la kuhudumia viwanda vidogo nchini (SIDO) wanatengeneza tera la miguu mitatu. "Ndani yake zitakuwa na friji dogo, brenda na sehemu za kuonesha mazao. Mtu ataweza akaihamisha au akakaa sehemu moja ya kudumu. Pia tela hizo zitakuwa na 'solar panel' kwa ajili ya kuifanya kazi hiyo. Tunaanza kugawa kwa ajili ya viwanda" alisema Waziri Bashe.

Aidha, serikali ilitoa rai kwa vijana wajitokeze kwa wingi kuchukua pikipiki hizo kwasababu ni chachu ya maendeleo katika jamii na taifa kiujumla. Kupitia pikipiki hizo zitawasaidia kujikwamua kimaendeleo kutoka hali ya chini kimaisha hali hali ya juu. Kwa sababu kutokana na teknolojia waliyoitumia kutengeneza pikipiki hizi ni ya kisasa zaidi.

# Nanenane muhimu kujifunza Kilimo na Ufugaji bora



Na. Rahma Abdallah na Jackline Patrick

MAADHIMISHO ya siku ya wakulima Nanenane ni maonesho ya muhimu ambayo humuwezesha mwananchi kujifunza katika kilimo, ufugaji pamoja na uvuvi. Maonesho hayo ni mahususi kwa kila mtanzania katika kuzalisha mazao yenye tija kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Hayo yalizungumzwa na Diwani wa Kata ya Kikombo, Emmanuel Manyono alipokua akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maonesho ya kimataifa ya Nanenane jijini Dodoma.

Manyono alisema kuwa maadhimisho hayo yanaleta tija kwa jamii na pia kuwapa wakulima elimu ya kilimo na ufugaji bora. "Maonesho haya yamekua yakileta tija, kumekua na mafunzo mengi yakisaidia wakulima kuondokana na kilimo cha zamani na sasa kulima kwa kuzingatia kilimo cha kisasa. Kilimo cha kisasa kina mafanikio makubwa, mkulima analima shamba dogo linalotoa mazao mengi na bora. Hivyo, rai yangu wakulima wajifunze kulima kilimo cha kisasa. Wananchi wajitokeze katika maonesho ya Nanenane hapa Nzuguni kujifunza mbinu bora za kilimo cha kisasa na matumizi ya teknolojia za kilimo" alisema Manyono.

Pia alisema kuwa kuwepo kwa maonesho hayo kunaleta chachu kwa wakulima nchini kutokana na fursa zinazotolewa kwa wakulima wote katika uuzaji wa mazao kwa kunufaika zaidi na kilimo chao. Tofauti na mfumo wa kizamani ambao ulikua ukiwanyonya wakulima, aliongeza.

Akiongelea changamoto zinazowakabili wakulima, alisema ni uelewa na kufuata maelekezo ya wataalam kuhusu kilimo bora. "Maonesho ya Nanenane yanasaidia utoaji wa elimu kwa sababu wananchi wanaelimishwa huku wakiona kwa macho. Hivyo, maonesho haya yanaleta mabadiliko kwa mtu binafsi na taifa kwa ujumla. Hivyo, nawaomba wananchi wote kujitokeza kwa wingi katika mabanda hasa banda la Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa ajili ya kupata elimu ya kilimo bora" alisema Manyono.

Maadhimisho ya kimataifa ya Nanenane kanda ya Kata yalianza tarehe 1-8 Agosti, 2024 yakiongozwa na kaulimbiu isemayo 'Chagua viongozi bora wa Serikali za Mitaa kwa maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi'.

"Maonesho haya yamekuwa yakileta tija, kumekua na mafunzo mengi yakisaidia wakulima kuondokana na kilimo cha zamani na sasa kulima kwa kuzingatia kilimo cha kisasa. Kilimo cha kisasa kinamafanikio makubwa, mkulima analima shamba dogo linalotoa mazao mengi na bora"

# Serikali kuboresha viwanja vya maonesho ya Nanenane

Na. Moureen John

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amesema serikali itaendelea kufanya maboresho katika viwanja vya maonesho ya Nanenane ikiwa ni mkakati wa kuchangia ukuaji wa uchumi nchini.



*Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe*

Kauli hiyo aliitoa wakati wa uzinduzi maonesho ya kimataifa ya Nanenane kanda ya kati katika uwanja wa Nanenane Nzuguni jijini Dodoma.

Waziri Bashe alisema "Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo mwaka jana jijini Mbeya kwamba serikali ianze kufanya mabadiliko ya ujenzi kwa viwanja vya maonesho ya Nanenane. Kiwanja cha kwanza ni Nzuguni, Dodoma na Mwakangale, Mbeya katika hali ya kawaida tungesema tumehairisha shughuli za Nanenane mpaka tumalize hali ya ujenzi lakini tukasema Nanenane itaendelea na ujenzi utaendelea kwa wakati mmoja. Ujenzi umeanza wa uwanja huu na ujenzi huo utakuwa ni wa awamu tatu mpaka utakapokamilika na awamu ya kwanza ndio imeanza na ilikuwa shughuli ya kuondoa watu waliokuwa wamevamia eneo hili tunawahukuru sana wao wenyewe kwa hiari yao walikubali kuondoka kwasababu wanaamini eneo hili ni mali ya serikali" alisema Waziri Bashe.

"Serikali imeanza na ujenzi wa uzio, uwanja huu utakuwa na maeneo ya vipando, uwanja huu utakuwa na onesho la mifugo, uwanja huu utakuwa na maonesho ya shughuli za uzalishaji mwaka mzima. Lakini ndani ya uwanja huu kutakuwa na eneo la 'conference facility' na mikutano. Vilevile, kutakuwa na eneo la 'incubation centre' kwa ajili ya vijana wanaofanya teknolojia na hivi sasa shughuli za ujenzi zimeanza mpaka awamu zote zitakapokamilika. Serikali itatumia zaidi ya shilingi bilioni 40 kukamilisha miundombinu yote ya uwanja wa Nanenane Nzuguni Dodoma" alisema Waziri Bashe.

Aidha, alimtaarifu Waziri Mkuu wa Tanzania aliyekuwa mgeni rasmi kuwa baada ya kukamilisha viwanja vya Nzuguni na Mwakangale wataenda hatua ya pili ambayo itahusisha viwanja vya Morogoro, Arusha, Lindi na Tabora.

> "Serikali itatumia zaidi ya shilingi bilioni 40 kukamilisha miundombinu yote ya uwanja wa Nanenane Nzuguni Dodoma hatua ya pili itahusisha viwanja vya Morogoro, Arusha, Lindi na Tabora"

# Wafanyabiashara wanufaika na ufunguzi wa Nanenane na uzinduzi wa SGR




Na. Rahma Abdallah

WAFANYABIASHARA wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma wamenufaika kutokana na ufunguzi wa maonesho ya siku ya Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya Nanenane Nzuguni jijini Dodoma pamoja na ufunguzi wa treni ya kisasa ya mwendo kasi inayotumia umeme (SGR), ufunguzi huo uliofanyika Kata ya Kikuyu Kusini jijini Dodoma.

Hayo yamezungumzwa na wafanyabiashara wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma mapema jana katika ufunguzi wa maonesho ya Nanenane pamoja ufunguzi wa Treni ya kisasa inayotumia umeme (SGR).

“Nashukuru Mungu mimi nikiwa kama mfanyabiashara wa chakula nimenufaika sana kwa sababu watu ni mengi sana hatuna budi kumenya viazi vingi ili wateja wetu wanapokuja kukuta kila kitu kiko vizuri pia kupitia ufunguzi huu sisi kama wafanyabiashara tumepata fursa kwasababu kabla ya uzinduzi huu biashara haikuwa nzuri kabisa kwa sababu ya ukosefu wa watu (wateja) lakini kwa kupitia uzinduzi huu tumechangamkia na kufanya biashara” alisema mfanyabiashara Emmanuel Edward.

Nae, mfanyabiashara wa chombo cha moto (dereva wa bajaji) anaefahamika kwa jina la Noel Yonah alisema “siku ya leo ni siku nzuri sana hasa kwetu sisi wafanyabiashara wa vyombo vya moto kwasababu watu ni wengi sana inafikiwa wakati mpaka mimi mwenyewe kama mfanyabiashara nachoka kubeba au kupakia wateja. Yaani wateja wananifata lakini mimi nawaambia mimi siendi. Kwahiyo, leo tumenufaika sana tunatamani kila siku biashara iwe kama ya leo”.

Kwa upande wa mkazi wa Dodoma, Mariam Alex alisema kuwa biashara ni nzuri. “Leo ni siku ya pesa kama unavyo ona watu ni wengi tena wananchi wa hapa hapa Tanzania. Mimi nikiwa kama mfanyabiashara ninae uza hizi bendera ndogo za Taifa letu la Tanzania nimepata pesa nyingi kwasababu kila mtu ananunua bendera ili aonekane ni mwananchi halali wa Tanzania. Kwahiyo, biashara yangu imeenda vizuri kwasababu watanzania wenzangu wameniunga mkono namshukuru Mungu, lakini pia nisiwe mchoyo wa fadhila kuwashukuru na watanzania wenzangu” alisema Alex.

Aliongeza kwa kusema kuwa uzinduzi na ufunguzi ni chanzo cha fursa. Sisi tukiwa kama wananchi kwasababu, unaweza kubuni na kuanza biashara yako kidogo kidogo na mwisho kuwa mfanyabiashara mkubwa. “Kwahiyo, sisi kama wananchi hasa vijana tuache tabia ya uvivu na tujaribu kujishughulisha ili tuweze kukidhi mahitaji yetu” alisema Alex.

# Maandalizi ya Nanenane 2024 Dodoma yapamba moto



Na. Flora Nadoo

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Alhaj Jabir Shekimweri ampongeza Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka alama katika maboresho ya miundombinu ya maonesho ya Nanenane Kanda ya Kati Dodoma.

Kauli hiyo aliitoa mjini Dodoma alipokuwa akiongelea maandalizi ya maadhimisho ya sherehe za Nanenane zinazofanyika katika viwanja vya Nanenane Nzuguni.

Alhaj Shekimweri alisema kuwa mwaka jana Rais wakati akiahirisha maonesho ya Nanenane Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwenye Uwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya alielekeza maboresho ya viwanja vya Nanenane.

Alisema kuwa viwanja viwili vimechaguliwa kuanza kufanyiwa ukarabati. Alisema kuwa Waziri wa Kilimo, Husein Bashe na viongozi wa Wizara chini ya Katibu Mkuu wa wizara ya Kilimo Gerald Mweli wameanza ukarabati wa viwanja hivyo. "Tumeanza kufanya kazi mbalimbali, miongoni mwa kazi hizo ni pamoja na udhibiti na uendeshaji wa uwanja kwa kujenga uzio, kujenga sehemu ya upashanaji habari (Information Centre).

Shekimweri alisema kwenye maonesho hayo ya Nanenane kutakuwa na mitambo ya kuchakata kwenye kilimo kama vile trekta, pawatila na nyingine nyingi. Wazalishaji wa vifaa hivyo watakuwepo, kila anayehusika na tasnia ya kilimo atakuwepo ili wananchi waweze kuona, kujifunza, na kuchangamkia fursa zinazotokana na shughuli za maonesho.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma alisema kuwa anategemea kuwa na watu wengi sana watakaoshiriki maonesho hayo ikiwemo taasisi za kimataifa pamoja na nchi za jirani zisizopungua tano na taasisi 45 zimethibitisha kushiriki katika maonesho hayo.

Aliongeza kuwa Dodoma ni kanda pekee yenye paredi ya mifugo kutokana na maonesho hayo masoko ya wakulima yanaweza yakaanza kuunganishwa nje ya nchi na kwa namna hiyo wakulima watapata thamani kubwa sana kutokana na kazi kubwa wanayoifanya na jasho wanalolitumia.

Maadhimisho ya Nanenane mwaka 2024 yanaongozwa na kaulimbiu isemayo 'Chagua viongozi bora wa serikali za mitaa kwa maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi'.

"Kwenye maonesho hayo ya Nanenane kutakuwa na mitambo ya kuchakata kwenye kilimo kama vile trekta, pawatila na nyingine nyingi. Wazalishaji wa vifaa hivyo watakuwepo, kila anayehusika na tasnia ya kilimo atakuwepo ili wananchi waweze kuona, kujifunza, na kuchangamkia fursa zinazotokana na shughuli za maonesho"

# Matrekta 600 kwenda kwa wakulima




Na. Anna Stanley

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua Matrekta 600 pamoja na zana za kilimo kwenda kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini.

Hayo yalifanyika katika viwanja vya Nanenane wakati wa maadhimisho ya kilele cha Nanenane kitaifa Nzuguni, Dodoma, mwaka huu 2024. Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua kiwanda hicho cha kuunganisha Matrekta ili kurahisisha shughuli zote za kilimo kwa wakulima nchini hii itasaidia kutoagiza tena Matrekta kutoka nchi za nje.

"Nifahari yangu kwamba leo tumeweza kuzindua matrekta 600 kwenda kwa wakulima katika maeneo mbalimbali lakini mbali ya kununua matrekta yale kiwanda cha kuunganisha matrekta sasa kipo Dodoma hapa Tanzania ambapo hatutaagiza tena matrekta kutoka nje ya nchi na kabla ya 2030 tutakuwa tumepeleka matrekta 10,000 na Pawatila 10,000 kwa wakulima mbalimbali nchini, Hili litaenda kutekelezwa kwasababu kiwanda tayari kipo Dodoma hapa Tanzania" alisema Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Aidha, kwa upande mwingine Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alimpongeza na kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa na maono makubwa na kuweza kuyatekeleza.

"Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kipekee mimi naomba nikushukuru na kukupongeza wewe zaidi tumshukuru Mungu kwa ajili yako kwa kuweza kubahatika na maono makubwa na unaweza kuyatekeleza,
Sisi tunajivunia kutokana na uthubutu wako wa kutekeleza mambo makubwa sana na yenye kuleta maendeleo kwa Taifa letu la Tanzania, sasa Kanda ya Kati Dodoma na Singida tunaongea lugha tofauti tunasema,kanda ya kati itatosheleza mafuta Tanzania, Kanda ya kati italisha nchi nzima ,kanda ya kati itafanya uchumi wa nchi hii kubadilika na kukua,

Hayo yametokana na maono uliotufunulia na ukaanza kutuwekea miradi ya umwagiliaji na mambo makubwa katika sekta ya kilimo hakika tunakushukuru sana " alisema Senyamule

> "Mbali ya kununua matrekta yale kiwanda cha kuunganisha matrekta sasa kipo Dodoma hapa Tanzania ambapo hatutaagiza tena matrekta kutoka nje ya nchi na kabla ya 2030 tutakuwa tumepeleka matrekta 10,000 na Pawatila 10,000 kwa wakulima mbalimbali nchini, hili litaenda kutekelezwa kwasababu kiwanda tayari kipo Dodoma hapa Tanzania"

# CCM yampongeza Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Utekelezaji Ilani

Na. Dennis Gondwe

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Pongezi hizo zilitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa CCM Tanzania Bara, John Mongela alipotoa salamu za CCM katika kilele cha maonesho ya Nanenane kitaifa, Nzuguni Dodoma.

Mongela alisema “Ilani ya CCM ina kurasa 308, kurasa 33-56 zinaelezea sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Leo mimi ni shahidi kwamba utekelezaji wa Ilani unafanywa kwa kiwango cha juu sana, tumpongeze Rais na serikali yake. Chini ya uongozi wako ni kazi kubwa inatambulika kwenye sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi”.

Aidha, aliahidi CCM kuendelea kufanya kazi karibu na serikali ili wananchi wapate maendeleo zaidi.

Akitoa salamu kutoka kwa mabalozi wa nchi za nje, Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Michael Battle alisema kuwa washirika wa maendeleo wanaunga mkono juhudi za Tanzania katika kukuza sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi hasa ushiriki wa wanawake na vijana.

Alisema kuwa Serikali ya Marekani itaendelea kuchangia katika Kilimo cha Tanzania kupitia mpango wa Feed the Future unaofadhiliwa na USAID.

Aidha, alimhakikishia Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Marekani na washirika wake wapo tayari kuitangaza Tanzania kuwa imefunguka kibiashara. “Mungu akupe nguvu na hekima ya kuongoza Tanzania” alimalizia Balozi Battle.

# Marufuku uuzaji wa maziwa kwenye ndoo na chupa za maji

Na; Rahma Abdallah

BODI ya Maziwa Tanzania iliyoanzishwa na serikali kwa sheria namba nane mwaka 2004 ikiwa na jukumu la kusimamia sekta ya maziwa nchini imekataza uuzaji wa maziwa kwenye ndoo pamoja na machupa ya maji kwani siyo salama kwa watumiaji.

Hayo yalizungumzwa na Afisa Teknolojia wa Bodi ya Maziwa Tanzania, Rajilan Hilal alipokua akizungumza kwenye siku ya pili ya maonesho ya Nanenane akiwa na waandishi wa habari pamoja na wananchi wa jijini Dodoma.

Kusema kuwa wauzaji wa maziwa wanaotumia ndoo pamoja na chupa za maji wanatakiwa kuacha mara moja.

Mfumo wa uuzaji wa maziwa kwa kutumia ndoo chupa za maji pamoja na madumu tunaupiga marufuku sisi tukiwa kama mamlaka kwa sababu haturuhusu mtu yeyote kutumia zana za namna hii kubebea maziwa kwa sababu zana hizo ambazo wanatumia mfano chupa za maji siyo salama hutumika na mtu usiye mfahamu’’

Aliongeza kwa kusema kuwa vipo vyombo maalum na vyenye usalama kwa ajili ya kuhifadhi na kufungashia maziwa na ambavyo vinaosheka kwa urahisi ni tofauti na chupa za maji pamoja na madumu. Hivyo basi ni makosa kisheria kutumia zana hizi katika kuhifadhi na kufungashia maziwa siyo salama kwa afya.

Lakini pia mkazi wa Kata ya Miyuji Rehema Yusuph alisema ‘’wauzaji wa maziwa kwenye mitaa yetu wamekuwa na tabia zisizofaa hata kidogo kwa sababu kwanza maziwa

yanaongezwa maji yaani unanunua maziwa kwa bei ghali alafu unakuta yameongezwa maji yaani unakunywa maziwa lakini husikii ladha ya maziwa. Kwahiyo mimi napenda kuwaasa au kuwashauri wote ambao wanatabia kama hizi waziache” alisema Rehema Yusuph.

Pia muuzaji wa maziwa, Baraki Hussein alisema ‘’ asilimia kubwa ya wauzaji wa maziwa tunahiyo tabia ya kuongeza maji kwenye maziwa pia kuokota chupa zilizoishiwa maji na kufungashia maziwa hii inatokana na kutonunua zana nzuri zilizo andaliwa kwa ajili ya kufungashia maziwa ili kuweza kuboresha huduma kwa wateja wetu na kukuza biashara zetu.

Hivyo wafanyabiashara wote wanao jishughulisha na biashara ya uuzaji wa maziwa wanatakiwa kuwa na vyombo maalumu kwa ajili ya kuhifadhi pamoja na kufungashia maziwa ili kulinda afya za watumiaji maziwa hayo yanayo uzwa. Pia kuacha tabia ya kuongeza maji kwenye maziwa mnaondoa virutubisho vilivyopo kwenye kimiminika hicho. Hivyo mnatakiwa kuwa waaminifu katika biashara zenu ili kuziboresha pamoja na kuzilinda.

# Kaulimbiu ya Nanenane 2024 yaleta tija katika Jamii

Na. Fadiga James

KAULIMBIU ya maonesho ya Nanenane mwaka 2024 isemayo ‘Chagua viongozi bora wa serikali za mitaa kwa maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi’ imetajwa kuwa na tija katika jamii.

Kauli hiyo ilitolewa na mkazi wa Kata ya Ng’hong’ona Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Nyemo Msambili leo tarehe Mosi Agosti, 2024 katika uzinduzi wa maonesho ya kimataifa ya Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya Nanenane, Nzuguni, Dodoma.

Msambili aliiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kaulimbiu ya maonesho ya Nanenane mwaka 2024 isemayo ‘Chagua viongozi bora wa serikali za mitaa kwa maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi’ inafanyiwa kazi vizuri. Aidha, aliiomba serikali kuweka watu sahihi watakaosimamia uchaguzi wa serikali za mitaa.

“Kaulimbiu ya maonesho ya Nanenane mwaka 2024 ina tija na maana kubwa katika jamii zetu, ukiangalia huu ni mwaka wa uchaguzi. Hivyo,



serikali imeanza kutusihi mapema kuweza kuchagua viongozi bora wa serikali za mitaa ambao watatuletea maendeleo katika sekta hizo na mimi ningependa tu kuwashauri ndugu zangu, kuwa tusifanye makosa kwenye uchaguzi. Hivyo, tuchague viongozi bora” alisema Msambili.

Aliongeza “ningependa kuiomba serikali iweze kuteua watu ambao wataenda kusimamia vizuri uchaguzi na kuhakikisha haki inatendeka kwenye uchaguzi huu wa serikali za mitaa”.

# Watanzania tumieni haki yenu ya kikatiba, nendeni mkahahakiki majina yenu kwenye daftari: Waziri Mkuu Majaliwa

Na. Francisca Mselemo

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa amewataka watanzania kutumia haki yao ya kikatiba ya kupiga kura na kwamba ili waweze kutumia haki hiyo wanatakiwa kuhakiki majina yao katika daftari la kudumu la wapiga kura.




*Waziri Mkuu akiwa katika Ufunguzi wa Maonesho ya Nanenane, Nzuguni-Dodoma*

Majaliwa aliyasema hayo Agosti 01, 2024 wakati akifungua maonesho ya kimataifa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi maarufu kama maonesho ya Nanenane yanayofanyika katika viwanja vya Nzuguni vilivyopo Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Majaliwa alisema kuwa tayari Serikali imeshazindua uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura na kwamba katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Geita na Kagera uboreshaji umeanza. Hivyo wananchi wawe tayari, itakapofika kwenye mikoa yao waende kuhakiki majina, kama hayapo, wajiandikishe ili wakati wa kupiga kura wote waweze kupiga kura.

Akisisitiza kuhusu umuhimu wa kufanya uhakiki na kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura, Majaliwa alisema "Mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi wa serikali za mitaa, kila mtanzania ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa, tutumie vema haki yetu ya kikatiba. Twende tukahakiki majina yetu kwenye daftari, tuhakikishe yamo ili isije ikatokea imefika siku ya kupiga kura, mtu unakwenda kituoni unatafuta jina lako hulioni unaanza kulalamika. Mimi jina langu silioni, kumbe wakati wa kuhakiki majina hukwenda kuhakiki.Wote tuhakiki majina yetu na kwa wale ambao wakati wa uandikishaji hawakuwa wamefikisha miaka 18, sasa wamefikisha wakajiandikishe, waliohamia maeneo mengine, nao wakarekebishe taarifa zao ili waweze kupiga kura katika maeneo wanayoishi sasa''.

Wakati huohuo, Majaliwa amewahakikishia watanzania kuwa sasa wanaweza kulima na kufuga bila kuwa na wasiwasi kwasababu soko lipo.

"Wakulima wa mahindi msiwe na mashaka limeni masoko yapo, kazi tuliyonayo wananchi ni kulima, kuzalisha lakini tuzingatie kilimo cha kisasa. Tanzania tunakwenda kwa kasi, watanzania fanyeni maamuzi ya kulima, kufuga, kuvua, Serikali imeweka mpango mzuri, itawafikia hata vijijini" alisisitiza Majaliwa.

Kadhalika Majaliwa aliwataka wafugaji kubadilika wafuge maeneo maalum, wasitembeze mifugo umbali mrefu kwa kufanya hivyo inapungua thamani.

Sambamba na hayo, Majaliwa aliwataka maafisa ugani kutumia mifumo ya kidigitali kuwafikia wakulima.

"Tumieni mifumo ya kidigitali muwafikie wakulima kokote waliko, muwashauri, muwaambie namna nzuri ya kulima, namna nzuri ya kutunza mazao yao na namna nzuri ya kupata masoko. Wasaidieni wakulima namna ya kupata mitaji kwenye taasisi zetu" alisema Majaliwa.

# Wananchi wafurahishwa na elimu waliyoipata Banda la TANROADS maonesho ya Nanenane



*Wananchi wakipewa elimu katika banda la TANROADS, Nzuguni-Dodoma*

Na. Janeth Gerald

WANANCHI na Wakazi wa Mkoa wa Dodoma na vitongoji vyake wamefurahishwa na elimu kuhusu masuala mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu ikiwemo barabara, madaraja, viwanja vya ndege inayotolewa na (TANROAD) katika banda la maonesho ya kitaifa ya wakulima Nanenane yanayoendelea kwenye viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma.

Mchezaji wa zamani wa timu ya taifa na Simba, Mtemi Ramadhani alisema ameridhishwa na elimu aliyoipata kutoka kwa wataalamu baada ya kutoka kuelezwa maendeleo ya miradi ya barabara za Handeni- Kibirasi- kwa Mtoro- Singida.

"Nilitaka kufahamu kuhusu barabara hizo maana nimekuwa nikipita zilikuwa hazipo katika hali nzuri na nyingine zilishaanza kujengwa, nashukuru nimeridhishwa na changamoto zilizopo" alisema Mtemi.

Naye Mwandishi mkongwe na msemaji wa zamani wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Badra Masoud alitaka kujua viwango vya ubora wa barabara na malighafi zake. Masoud, ambaye kwa sasa ni mkulima wa mazao ya mahindi na alizeti, alisema amekuwa akitumia barabara mara kwa mara kusafirisha mazao hayo baada ya kuvuna.

"Nimeridhishwa na elimu inayotolewa pale kwenye kitengo chenu cha utafiti na maabara, wamenieleza namna wanavyopima udongo, lami, kokoto, mchanga na malighafi nyingine za utengenezaji wa barabara, kwa kweli mnafanya kazi nzuri asanteni" alisema Masoud.

Kwa upande wake Mhandisi Arnold Masaki wa TANROAD alisema kuwa katika banda lao wanatoa elimu ya uhifadhi wa barabara kwa matumizi ya kibinadamu kama ujenzi wa nyumba za kuishi, maduka na vibanda vya biashara, kulima mazao mbalimbali.

"Ni kosa kutumia hifadhi ya barabara na mtu atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria iliyopo namba 13 ya mwaka 2007 kifungu cha 29 inayoonesha wazi eneo la hifadhi ya barabara kuu na za mikoa ni urefu wa mita 30 kila upande kuanzia katikati ya barabara" alisema Masaki.

Masaki aliongeza kuwa, athari za kuingia kwenye hifadhi ya barabara ni pamoja na kusababisha ajali kwa watumiaji wa barabara kutokana na kupunguzwa kwa upeo wa kuona, mmomonyoko wa ardhi pembezoni mwa barabara kutokana na maji yatakayotiririka kutoka kwenye nyumba zilizojengwa. Ajali kwa watoto ambao wanaweza kucheza mbele ya nyumba zao, kuziba kwa mifereji inapitisha maji ya mvua, afya za wakazi kudhurika kutokana na makelele ya magari na wananchi kupata hasara kwa kubomolewa nyumba zao wakati wa ujenzi wa barabara husika.

Pia amesema wananchi wameelimishwa juu ya upimaji wa mizigo kwenye mizani ya magari yanayobeba mizigo kutoka mkoa mmoja na hata kwenda nje ya nchi.

# Wataalamu waaswa kupeleka teknolojia ya mifugo na Uvuvi vijijini




Na. Janeth Gerald

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule amewaasa wataalamu wa sekta za Mifugo na Uvuvi kupelekea na kufundisha teknolojia za sekta hizo vijijini ili kuwapa wafugaji elimu ya kutosha kuhusu ufugaji wa kisasa kwa lengo la kuleta tija.

Alizungumza, Agosti 4,2024 mkoani Dodoma alipotembelea kwenye Maonesho ya Kilimo ya Kitaifa (Nanenane) 2024 yalifanyika kitaifa Mkoani humo, Senyamule amesema wataalamu wahakikishe teknolojia za kisasa zinawafikia wadau wote wa Mifugo na Uvuvi, hususani maeneo ya vijijini. "Wataalamu wachukue hatua ya kwenda kwenye Makundi ya wafugaji ili kwenda kuwaelimisha kuhusu teknolojia mpya ya ufugaji na kuhakikisha inawafikia" amesema Senyamule

Senyamule alisema sekta binafsi pia nimepokea mabadiliko hayo ya kiteknolojia, hususani upande wa vijana wa Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) ambao wanatumia teknolojia hizi Kama ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba. Aidha, alisema serikali ya Awamu ya Sita ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya mapinduzi makubwa Sana katika sekta za Mifugo na Uvuvi kwani ameshuhudia teknolojia mbalimbali na nzuri katika mabanda ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Pia, ametoa wito kwa wadau wote wa Mifugo na Uvuvi kutumia fursa hii ya Maonesho haya ya Nane Nane ili kuweza kujifunza na kupata ufahamu juu ya teknolojia za kisasa za Mifugo na Uvuvi.

# Kaulimbiu ya Nanenane 2024 yaletatija katika Jamii

Na. Fadiga James

KAULIMBIU ya maonesho ya Nanenane mwaka 2024 isemayo 'Chagua viongozi bora wa serikali za mitaa kwa maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi' imetajwa kuwa na tija katika jamii.

Kauli hiyo ilitolewa na mkazi wa Kata ya Ng'hong'ona Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Nyemo Msambili tarehe Mosi, Agosti, 2024 katika uzinduzi wa maonesho ya kimataifa ya Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya Nzuguni, Dodoma.

Msambili aliiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kaulimbiu ya maonesho ya Nanenane mwaka 2024 isemayo 'Chagua viongozi bora wa serikali za mitaa kwa maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi' inafanyiwa kazi vizuri. Aidha, aliiomba serikali kuweka watu sahihi watakaosimamia uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Kaulimbiu ya maonesho ya Nanenane mwaka 2024 ina tija na maana kubwa katika jamii zetu, ukiangalia huu ni mwaka wa uchaguzi. Hivyo, serikali imeanza kutusihi mapema kuweza kuchagua viongozi bora wa serikali za mitaa ambao watatuletea maendeleo katika sekta hizo na mimi ningependa tu kuwashauri ndugu zangu, kuwa tusifanye makosa kwenye uchaguzi. Hivyo, tuchague viongozi bora" alisema Msambili.

Aliongeza "ningependa kuiomba serikali iweze kuteua watu ambao wataenda kusimamia vizuri uchaguzi na kuhakikisha haki inatendeka kwenye uchaguzi huu wa serikali za mitaa".

# Utumiaji wa Maziwa Ghafi Nchini

Na. Jackline Patrick

WANANCHI wameshauriwa kutumia maziwa salama na kuepukana na kutumia maziwa yanayouzwa katika chupa mtaani ili kulinda afya zao.

Ushauri huo ulitolewa na Afisa Teknolojia wa Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB), Rajilan Hilal wakati wa mahojiano maalum na mwandishi wa habari hii katika banda la bodi hiyo lililopo Nanenane jijini Dodoma.


Hilal alisema "nashauri watu kutumia maziwa ghafi ambayo ni yogati, siagi, jibini na mtindi. Mamlaka inatekeleza jukumu la uratibu wa shughuli za wadau. Wadau wasajiliwe maana sheria inataka wasajiliwe ili kuhamasisha bidhaa za maziwa".

Alisema kuwa kila mwaka ifikapo mwezi Septemba, yanafanyika maadhimisho ya unywaji maziwa nchini. Bodi yake hutoa hamasa ya unywaji maziwa shuleni, katika ofisi za umma na sekta binafsi. "Bodi imefanikiwa kuhamasisha unywaji wa maziwa, mpaka sasa nchini tumefikia lita 67.5 kwa mtu. Kwa mwaka jana tulikua na lita 62, juhudi zinaendelea kufanyika" alisema Hilal.

Afisa Teknolojia alisema kuwa zipo fursa nyingi katika uzalishaji maziwa. "Watu waingie katika tasnia ya maziwa, kuna fursa za uwekezaji. Uwekezaji katika pembejeo, uwekezaji katika vifungashio, uwekezaji wa viwanda vya maziwa, uwekezaji wa mashamba ya ng'ombe, wafugaji wahakikishe wanafuga mifugo yao katika utaratibu ili kuondokana na maziwa yasiyo salama" alisisitiza Hilal.

Aidha, aliwataka wafugaji wote wawe waaminifu. "Wamama wanatumia maziwa ya ngo'mbe kunyonyeshea watoto kwa sababu maziwa ni chakula bora na pia ni mlo kamili. Maziwa yana viini lishe vyote vinavyomuwezesha mtoto kukua vizuri. Tunahamasisha utumiaji maziwa utolewe shuleni ili uweze kukuza watoto na kuepuka changamoto kubwa ya udumavu wa akili" aliongeza Hilal.

Bodi ya Maziwa Tanzania ni mamlaka ya serikali iliyoanzishwa kwa sheria Namba Nane ya Mwaka 2004 kwaajili ya kusimamia sekta ya maziwa nchini, wadau ambao wanatekeleza majukumu yao ambao ni wafugaji, wachukuzi, wasindikaji na watumiaji maziwa.



# Tanzania kupiga hatua kimataifa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi




*Balozi wa Marekani nchini Tanzania, picha na mtandao*

Na. Emmanuel Lucas


TANZANIA kutarajia kupenya kimataifa, hilo limethibitishwa na Balozi wa Marekani Michael Battle, akiazimia Marekani kuitangaza Tanzania katika sekta ya kilimo katika kilele cha maadhimisho ya siku ya kilimo, mifugo na uvuvi, Nanenane 2024 kitaifa na kanda ya kati yaliyofanyika katika viwanja vya Nanenane, Nzuguni-Dodoma.

Akitoa salamu kutoka kwa mabalozi wa nchi za nje, Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Michael Battle alisema kuwa washirika wa maendeleo wanaunga mkono juhudi za Tanzania katika kukuza sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi hasa ushiriki wa wanawake na vijana.

Alisema kuwa Serikali ya Marekani itaendelea kuchangia katika Kilimo cha Tanzania kupitia mpango wa Feed the Future unaofadhiliwa na USAID.

Aidha, alimhakikishia Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Marekani na washirika wake wapo tayari kuitangaza Tanzania kuwa imefunguka kibiashara. “Mungu akupe nguvu na hekima ya kuongoza Tanzania” alimalizia Balozi Battle.






**JARIDA HILI LIMETOLEWA NA**

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**



**S.L.P 1249 DODOMA, TANZANIA**

**Baruapepe: cd@dodomacc.go.tz**

**Tovuti: www.dodomacc.go.tz**